MATOKEO YA UCHAGUZI YALETA MSHANGAO

HADI TULIPOKUWA tukienda mitamboni, matokeo ya viti vya ubunge na vya udiwani kote mkoani Pwani yalikuwa yanaendelea kutangazwa. Katika viti vinne vya ubunge katika wilaya ya Mombasa, wabunge wawili wa zamani wamerudishwa, Mbunge mmoja wa zamani alishindwa na Mbunge mmoja mpya akateuliwa katika Mombasa Maghribi.

Katika mvutano mkubwa wa uchaguzi katika Mombasa ya Kati, Waziri Mdogo wa Wafanya kazi, Sheriff Nassir A. Taib aliendelea kuonyesha umaarufu wake baada ya kumbwaga mpinzani wake mkubwa. Bw. Mohammed Jahazi kwa jumla ya kura 11,828. Bw. Jahazi alipata kura 11,317.

Hii ni mara ya tatu kwa Bw. Nassir kumuangusha Bw. Jahazi kwani kutoka uchaguzi wa 1974, Waziri Mdogo huyo amekuwa akihifadhi kiti hicho. Mgombea uchaguzi mwingine wa kiti hicho, Bw. Odongo Ochola alipata kura 326 pekee.

Bw. Abdallah Ndovu Mwidau alionyesha ujasiri wake kwa kipindi cha pili wakati alipomuangusha tena mpinzani wake, Bw. Khalef Salim Mwavumo katika kukihami kiti cha Mombasa Kusini. Bw. Mwidau alinyakuwa kura 6,960 hali Bw. Mwavumo akapata kura 3,767 na Joseph Okoth Waudi akanyakuwa kura 3,725.

Kama kawaida, kiti cha Mombasa Kaskazini kilikuwa cha mapambano kwani aliyekuwa Chief Whip na Mbunge wa Sehemu hiyo kwa vipindi viwili, Bw. Said Hemed Said alishindwa na Bw. Ibrahim Abdallah Mwaruwa kwa kura 63. Bw. Mwaruwa alijinyakulia kura 10,490 na Said Hemed akapata 10,427.

Bw. Soud Machele aliyegombania kiti hicho pia, alijipatia kura 788; Bw. W. Mutunga akapata 299 na C. Farrah akajipatia kura 288 pekee. Bw. Mwaruwa alikuwa Mbunge wa Sehemu hiyo kabla ya kuangushwa na Bw. Hemed wakati wa uchaguzi wa 1974.

Kiti ambacho kiliachwa wazi na aliyekuwa Mbunge wa Mombasa Magharibi, Bw. David Kioko kilitetewa na wagombea wapatao 14 na mshindi aliyejinyakulia kiti hicho alitangazwa kama Bw. J. K. Kiliko aliyekong'oa jumla ya kura 4,493 za wakazi wa Mombasa Magharibi. Alifuatwa karibu na aliyekuwa Mbunge wa eneo hilo 1974, Bw. Ferdinand Mwaro aliyejinyakulia kura 4,175.

MZAMIL

Wananchi wa Lamu Mashariki wamekataa kubadilisha kwani aliyekuwa Mbunge wa kipindi kilichopita, Bw. Mzamil Omar Mzamil aliweza kuwashinda wapinzani wake wawili, Somo Abu Somo na Muhdhar Omar Saggaf kwa wingi wa kura. Bw. Mzamil alijipatia kura 5,278 hali Bw. Somo akajipatia 4,791 na Bw. Saggaf akapata 283 pekee.

MHARIRI wetu, *Abdulrahman Sheriff* **anatukusanyia vile uchaguzi mkuu wa wabunge ulivyokuwa katika mkoa wa Pwani.**

Tukigeuka Magharibi ya wilaya ya Lamu, Bw. Omar Twalib Mzee alikinyakuwa kiti kilichokuwa kimekaliwa na Bw. Abdulrahman Omar Cheka baada ya kupata jumla ya kura 3,468 na kumpita mpinzani wake James Ngigi Chege 3,002 na Michael Ndicu Ndungi 378. Bw. Cheka hakutetea kiti chake.

Mwanae Marehemu Juma Boy, Bw. Boy Juma Boy aliweza kujinyakulia kiti cha Kwale Kati baada ya kuwashinda wapinzani wake wawili, Bw. Mbwana Warrakah na Bw. Gidion Kioko. Bw. Boy alikung'uta kura 9,516; Bw. Warrakah 4,294 na Bw. Kioko 608.

Waziri wa Ushirika, Bw. Robert Stanley Matano alikihifadhi kiti chake cha Kwale Mashariki alipopita kwa kura 5,049 hali Bw. Mbarak Mwatsahu akanyakuwa 4,009 na Bw. A. A. Bidu akapata kura 3,343.

Naye Waziri Mdogo, Bw. Francis Bob Tuva aliweza kukabiliana na wapinzani watano na kuwashinda. Bw. Tuva alinyakuwa kura 5,090 hali mpinzani wake, Bw. Abubakar Badawy (Din) akapata kura 4,349, Bw. Tuva alipita katika kiti cha Malindi Kusini.

CHIBULE

Bw. Chibule wa Tsuma naye alikihifadhi kiti chake cha Kilifi Kusini alipopata kura 14,139 na kumshinda Bw. Daniel Runya aliyepata 1,842. Bw. Israel Lekwa Daiddo alirudi tena Bungeni baada ya kupata kura 16,120 na mpinzani wake mkubwa, Bw. Yuda Komora akapata 3,333 katika Tana Kusini.

Waziri Mdogo, Bw. Omar Soba amerudia tena kiti chake cha Tana Kaskazini baada ya kupata kura 5,520. Bw. Mwashengu wa Mwachofi alikihifadhi kiti cha Wundanyi baada ya kupata kura 9.950.

Naye Waziri wa Habari na Utangazaji, Bw. Eliud Mwamunga aliweza kuhifadhi kiti chake cha Voi alipopata kura 4,961.

Bw. C. Ondato alichukua nafasi ya tatu kwa kupata kura 4,149 na Bw. Josphat Mwai Karani akawa wanne (akiwana) kura 2,732. Matokeo mengine ya wagombea kiti hicho yalikuwa; S. R. D. Msechu (1452); Mauricce Ndoo (289); M. Ali Ali (232); M. Mwendar (333); M.P. Ofwona (350); A.M. Soud (450); P. Onyach (607); T. M. K. Chokwe (139) na O. G. Opondo (1070).

Bw. Kassim Bakari Mwamzandi aliye Waziri Mdogo na ambaye alikuwa Mbunge wa Kwale Mashariki kwa kipindi cha miaka 20 alikipoteza kiti chake wakati aliposhindwa kwa zaidi ya kura 5,000 na Bw. Ali Masoud Mwakileo.

Bw. Mwakileo aliye Mwenyekiti wa Kanu wilayani Kwale alijinyakulia jumla ya kura 12,442 akimshinda Bw. Mwamzandi aliyepata kura 6,467. Nafasi ya tatu Bw. Kiwango alipata kura 1,098 na Bw. K. M. Hamisi akashika mkia kwa kupata kura 303 pekee.

Wananchi wa Malindi Kaskazini waliamu kubadilisha wakati aliyekuwa Mbunge wa sehemu hiyo, Bw. Kasana Yeri alipoangushwa na Bw. J. K. Nzayi aliyekong'oa kura 2,527 na Bw. Yeri akapata kura 1,758. Bw. P.S. Mumbo akawa watatu kwa kupata kura 165 na Bw. A. A. Ahmed akapata kura 79 pekee.

Bw. Noah Katana Ngala aliendelea kuwachapa wapinzani wake vibaya wakati alipomshinda mpinzani wake wa pekee, Bw. Maurice Mboja kwa kura 13,026.

Bw. Ngala alikihifadhi kiti hicho cha Kilifi Magharibi baada ya wananchi 16,120 kumpa kura zao na Bw. Mboja kujipatia kura 3,094 pekee.

Habari nyingine za matokeo ya uchaguzi katika Pwani yalikuwa hatujayapata lakini inaonyesha wazi kuwa uchaguzi huu ulikuwa mgumu na usiotabirika. Kila Mpwani amefahamu kuwa mambo ya uchaguzi hayana dhihaka kwani matokeo yakitangazwa ya wagombea viti vya ubunge na udiwani katika wilaya ya Mombasa.

COASTWEEK pia itajaribu kuwaletea matokeo ya viti vya udiwani katika Mombasa lakini wakati tukikimbilia mtambuni, tumepata habari kuwa aliyekuwa Meya wa Mombasa, Bw. Rajab Sumba amekinyakuwa tena kiti cha wadi ya Majengo kwa kupata kura 4,366 hali mpinzani wake Bw. Mohammed Ali Qoyyan akapata kura 4,200. Zaidi juu ya uchaguzi usikose nakili yako wikii ijayo.

HAKI... MWANAMAMA huyu anatumia haki ya kupiga kura katika kituo cha Lohana kilichoko katika Mombasa ya Kati.
PICHA: NARENDRA PATEL

Pata Shika Katika ukumbi wa Jubilee mjini mombasa.

Hemedi Na Mwamzandi Nje!

HESABU... HAPA ni wakati wa kura za Mombasa ya Kati zilipokuwa zikihesabiwa na mshindi wa kiti hicho, Sheriff Nassir A. Taib amesimama nyuma akiwa chonjo.

HEKO.... MSHINDI wa kiti cha Mombasa Kaskazini, Bw. Ibrahim Abdallah Mwaruwa akipongezwa na Msimamizi wa uchaguzi wilayani Mombasa, Bw. Isaac Lukalo baada ya kushinda kiti hicho.

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO
SWAHILI CROSSWORD No. 171.

KWENDA KULIA:

3. District Officer.
4. Mahali panapoundwa vitu kwa mashine.
6. Ufupi wa "Do - ndoa mchele".
7. Mbegu ya mwembe
9. Aina ya ndege.
10. Kiungo cha maneno.
11. Kusanyeni pesa
13. Shahada ya elimu
14. Nusu ya "Dada".
15. Kula kiapo.
16. United Kingdom.

KWENDA CHINI:

1. Tosha, yenye faida
2. Jumla.
5. Mkokoteni
7. Aina ya mifupa katika mwili.
8. Kufunga ndoa.
12. Sikukuu ya Kiislamu.

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 170.

1. Grace Awori (Mrs), Sanduku La Posta 81383, MOMBASA.

2. Joseph Chalala, Sanduku La Posta 85696, MOMBASA.

3. Amina Noormohamed, Sanduku La Posta 90062, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 170.

KWENDA KULIA

1. MKALIMANI, 6. AU, 7. IDHINI, 8. FUA, 9. OA, 10. ALIA, 13. NK, 15. NA, 16. AAKA, 18. ZOROTA, 20. AU, 21. AUMA.

KWENDA CHINI

1. MFINYANZI, 2. ATHARI, 3. IUNDE, 4. AA, 5. NUNUA, 8. FOKA, 11. LAO, 12. ANOA, 13. NAAM, 14. MALIA, 17. KA, 19. TU.

JINA..

SANDUKU LA POSTA..............................

....

Shindano la Fumbo La Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri COASTWEEK Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatono tarehe Oct. 12. 1983, saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.